# MASOMO YA KIISLAM

**SHEIKH MUBARAK AHMAD H.A.**

**2002**

**Kimeenezwa na**
**Jumuiya ya Waislamu Waahmadiyya**
**S.L.P. 376 Dar es Salaam.**
**Tanzania**

# MASOMO YA KIISLAM

**Mwandishi - Sheikh Mubarak Ahmad H.A.**

**© Jumuiya ya Waislamu Waahmadiyya Tanzania**

**ISBN 9987 - 8932 - 4 - 4**

Chapa ya Kwanza ... ... ... ... 1939, nakala 1,000

Chapa ya Pili - Tisa ... ... ... ... nakala 36,000

Chapa ya Kumi ... ... ... ... 2002, nakala 5,000

Chapa ya Kumi na Moja ... ... ... ... 2010, nakala 5,000

**Kimeenezwa na Jumuiya ya Waislamu Waahmadiyya Tanzania**

**Kimechapwa na Ahmadiyya Printing Press**
**S.L.P. 376**
**Simu 2110473 . Fax 2121744**
**Dar es Salaam**

# YALIYOMO


1. Neno la Mbele ... 4
2. Dini ya Kiislam na Mwislam ... 5
3. Mwenyezi Mungu ... 6
4. Malaika ... 8
5. Unabii ... 9
6. Mtume Muhammad Mtukufu s.a.w. ... 10
7. Kurani Takatifu ... 13
8. Sunna na Hadithi ... 15
9. Dhambi ... 16
10. Wema ... 18
11. Sala ... 19
12. Kufunga Saumu ... 21
13. Kutoa Zaka ... 23
14. Kuhiji ... 24
15. Seyidna Ahmad a.s. ... 25
16. Siku ya Kiyama ... 26
17. Jihadi ... 28
18. Ndoa (Nikah) ... 30
19 Kuzaa ... 33
20. Maziko ... 34
22. Maneno ya Hekima ya Mtume Muhammad s.a.w. ... 35
21. Maagizo yanayomlazimu Kila Mwislam ... 38

بِسْمِ اللّٰهِ الرَّحْمٰنِ الرَّحِيْم

# NENO LA MBELE

Kwa rehema za Mwenyezi Mungu nchi nyingi za Afrika zimepata Uhuru na zilizobaki zitaupata baadaya muda si mrefu. Uhuru huu umewaletea wananchi uhuru wa kushika dini waipendayo na tunaona dalili nyingi za maendeleo mema upande wa Waislamu. Maelfu ya vitabu na mamilioni ya magazeti yamepigishwa chapa na kuenezwa na Jumuiya ya Ahmadiyya na watu wa Kenya, Uganda, Tanzania, Kongo na Mozambiki wameonyesha mahaba makubwa juu ya dini hii tukufu ya Islam. Kadiri ujuzi wa kusoma na kuandika utakavyozidi usomaji wa vitabu vya dini utazidi kiasi kile kile. Kwa hiyo tunafurahi kuona kazi iliyofanywa na Jumuiya hii imeonyesha tunda lake na kiu ya kupata elimu zaidi zaidi inaendelea uongezeka.

Ingekuwa bora zaidi kama kitabu hiki chenye manufaa sana kisomeshwe katika kila chuo cha Waislamu ili watoto wetu tangu udogo wao wawe na msingi imara wa dini yao wasipate kupotezwa na mtu ye yote. Kuieneza dini kati ya wale ambao hawajasilimu na kushika Uislamu vizuri-ndizo nguzo muhimu sana wakati huu. Umoja wa Mwenyezi Mungu na usawa na udugu wa wanadamu kama yalivyo fundishwa na dini ya Islamu yanafaa kuhubiriwa sana nchini kote. Mwenyezi Mungu atunufaishe na elimu ya mtungaji wa kitabu hiki, mwanachuoni maarufu-wa-Islamu, Maulana Sheikh Mubarak Ahmad H.A., ambaye amerejea Pakistan mwaka huu baada ya kuwatumikia wananchi kwa muda wa miaka 27. Amin.

Sheikh Muhammad Munawwar,
Mbashiri wa Islam.

Masjid Salaam,
P.O. Box 376, Dar es Salaam.
17 Juni, 1962.

# SOMO LA KWANZA
# DINI YA KIISLAM NA MWISLAM

I. Jina la dini yako ni nini?
Jina la dini yangu ni Islam.

2. Nani aliyetoa jina hili kwa dini yako?
Mwenyezi Mungu ndie aliyetoa jina hili kwa dini yangu.

3. Maana ya Islam ni nini?
Maana ya Islam ni kujitupa kwa Mwenyezi Mungu na kuingia katika amani.

4. Mradi wako nini kuwa dini yako inafundisha amani na kujitupa kwa Mungu?
Naam, dini yangu inawafundisha wafuasi wake wasimamishe amani katika dunia na kujitupa kwa Mwenyezi Mungu.

5. Nguzo za za Imani ni ngapi?
Nguzo za imani ni sita:-
   i. Kuamini Mwenyezi Mungu
   ii. Kuamini Malaika wake.
   iii. Kuamini vitabu vyake.
   iv. Kuamini mitume wake.
   v. Kuamini siku ya Kiyama.
   vi. Kuamini kadri ya Mwenyezi Mungu.

6. Nguzo za Kiislam ni ngapi?
Nguzo za Kiislam ni tano:-
   i. Kushuhudia: *Laa ilaaha illa-llah Muhammadur Rasulullah* yaani: Hakuna mwingine anayestahili kuabudiwa isipokuwa Mwenyezi Mungu, Muhammad ni Mjumbe wa Mwenyezi Mungu.
   ii. Kusali sala tano kila siku.
   iii. Kutoa Zaka.
   iv. Kufunga saumu mwezi wa Ramadhani.
   v. Kuhiji Kaaba.

7. Hakika ya Imani ni nini?
Hakika ya Imani si kukiri kwa ulimi tu, bali lazima kutenda pamoja na kukiri.

8. Niambie sharti za Imani.

Sharti za imani ni kukiri kwa ulimi na roho kuwa: *La ilaaha illa llah Muhammadur Rasuulullah,* Hapana Mungu ila Allah, Muhammad ni Mtume wa Mungu.

9. Wewe ni dini gani?
   Mimi ni Mwislam.
10. Nani aliyekupa jina hili la Mwislam?
    Mwenyezi Mungu ndiye aliyenipa jina hili.
11. Maana ya Mwislam nini?
    Maana ya Mwislam ni yule, anayekaa kwa amani na anafuata amri za Mungu, na amejitupa kwa Mwenyezi Mungu.

# SOMO LA PILI
# MWENYEZI MUNGU

1. Nani aliyekuumba?
   Mwenyezi Mungu ndiye aliniumba na ndiye aliyekiumba kila, kitu.
2. Mungu ni nani?
   Mungu ni Mtukufu na ndiye anayesifiwa kwa kila sifa njema, na yu mbali na sifa mbaya, Mwenye uwezo kabisa Mwumbaji, Mwenye kujua kila siri, Mwenye hekima, Mzima wa milele. Hasinzii wala Halali.
3. Je, Mungu ana mtoto?
   La, Mungu hana mtoto. sababu Yeye ndiye Mwumbaji si kiumbe na mtoto huzaliwa na kiumbe.
4. Mungu ni mmoia au watatu?
   Mungu ni mmoja tu hana mshirika.
5. Dalili gani ikuanoyeshayo kuwa Mungu ni mmoja?
   i. Lau kama miungu wangekuwa wengi wangaliharibu utaratibu wa dunia. Kwa sababu Mungu mmoja angalitaka wakati wa usiku uwe mchana, na mwingine angalitaka wakati ule uwe usiku, basi kwa hivyo wangalivunja utaratibutibu wa dunia.
   ii. Na lau kama wangekuwa wengi kwa hiyo itadhihirika kuwa Mungu ni mhitaji wa kusaidiwa, lakini yeye hana haja ya kusaidiwa, kwa sababu yeye anao uwezo juu ya kila kitu.
6. Dalili gani ikuonyeshayo kuwa Mungu yupo?

Nina dalili nyingi lakini sasa nitabainisha dalili mbili.

i. Kila kitu kinadhihirika kuwa kina mtengenezaji wake, inadhihiri kuwa kimetengenezwa na mmojawapo katika dunia. Hivi hivi sisi tunaona kuwa ulimwengu, ardhi, jua na mwezi, miti na matunda na vinginevyo vinayakinisha kuwa vina aliyevifanya. Na yeye ndiye Mungu.

ii. Na dalili ya pili ni shahada ya watu wa kweli. Yaani vitu vingi kwa sababu ya kushuhudia kwa watu vinakubaliwa; kama watu wengi hawakuona mji wa London, lakini wanakubali, kuwa mji wa London uko, kwa sababu ya kushuhudia kwa watu. Hivi hivi watu wengi wakweli kama mitume, wameshuhudia kuwa Mungu yupo.

7. Mungu yuko wapi?

   Mungu yuko kila pahali, na Kurani inasema: Mungu yupo pamoja nanyi po pote mlipo."

8. Je, Mungu anasema?

   Naam, Mungu anasema.

9. Mungu anasema na nani?

   Mungu anasema na wapenzi wake, wanaomfuata kwa nia safi na kutii amri zake sawasawa. Kama vile mitume na wale mawalii.

10. Je, sifa yake ya kusema imekwisha?

    Sifa yake ya kusema haikwisha, bali inaendelea mpaka siku ya Kiyama kama sifa zake zingine

11. Je, katika umati wa Muhammad s.a.w. yuko mtu aliyesema na Mungu?

    Naam yuko mtu aliyesema na Mungu naye ni Seyidna Ahmad katika mji wa Kadian bara Hindi. Na pia Seyidna Amirul-Muminin Khalifatul Masih wa pili aliyeitwa Hazarat Bashiruddin Mahmud Ahmad, Mungu awe radhi naye aliyeishi Rabwah, Pakistan, yeye pia alizungumza na Mwenyezi Mungu mara nyingi na akapokea habari za siri kutoka kwa Mwenyezi Mungu. Hata mawalii wa zamani waliokuwa baada ya Mtume s.a.w. kama Seyidna Abdul Quadir Jilani na maimamu wengine walipata kuzungumza na Mungu.

# SOMO LA TATU
# MALAIKA

1. Malaika ni nini?
   Malaika ni viumbe vya Mungu.
2. Kwa sababu gani Mungu amewaumba Malaika?
   Mungu aliwaumba Malaika katikati ya watu ili wafikishe amri zake kwa watu.
3. Je, mtu anaweza kuona Malaika kwa sura zao hasa?
   La, Malaika hawaonekani kwa sura zao hasa. Wanapoonekana na macho yetu wanaonekana kwa sura zingine.
   Kama vile alivyokuwa anakuja Malaika kwa Mitume kwa sura ya mwanadamu au sura nyingine.
4. Je, inayumkinika kwa Malaika kufanya kama watakavyo?
   Haiwezekani kwa malaika kufanya kama watakavyo. Bali "Wanafanya wanavyoamrishwa na Mwenyezi Mungu" (Kurani).
5. Malaika ni wangapi?
   Hakuna anayejua hesabu yao Ila Mungu.
6. Kazi gani za Malaika?
   Malaika wana kazi nyingi sana, lakini sasa nabainisha hapa baadhi ya kazi zao.
   i. Wao wanaleta maneno ya Mungu duniani
   ii. Wao ndio wanaochukua roho za watu wanaokufa.
   iii. Wao ndio wanaoleta adhabu kwa watu wabaya wanaokhalifu Mitume.
   iv. Na wao ndio wanaowasaidia waaminio na wapenzi wa Mungu.
   v. Na ndio wanaoingiza mapenzi katika roho za watu kukubali mitume.
   vi. Na wao ndio wanaohifadhi vitendo vya watu na kuviandika.
   vii. Na ndio wanaoingiza katika moyo wa mtu fikira ya kufanya wema.
7. Niambie majina ya Malaika unaowajua.
   Jibril, Mikail, Izrail, Israfil.
8. Shetani ni nani?
   Shetani ndiye anayeingiza katika mioyo ya watu nia ya kutenda

vitendo vibaya vya kila namna.

9. Je, inafaa kwa mtu kufuata mambo ya Shetani?
   Haifai mtu kufuata mambo ya Shetani na mtu akiyafuata atapigwa na Mungu na ataingizwa motoni.
10. Je, inafaa kufuata mambo ya Malaika?
   Naam, inafaa kufuata mambo ya Malaika na mtu akiyafuata atapelekwa peponi.

# SOMO LA NNE
# UNABII

1. Maana ya unabii ni nini?
   Maana ya unabii ni habari yenye cheo kikubwa au ubashiri utokao kwa Mungu.
2. Mtu anayepewa habari yenye cheo kikubwa kwa wingi anaitwaje?
   Anaitwa Nabii, Mtume, au Mjumbe wa Mungu.
3. Kwa sababu gani Nabii anaitwa mjumbe?
   Nabii anaitwa mjumbe kwa sababu Mwenyezi Mungu anamtuma kwa maneno Yake.
4. Kwa kusudi gani Mitume wanakuja duniani?
   Mitume wanakuja duniani ili kuwaongoza watu kwenye njia ya Mungu. Na kuwasuluhisha watu ili waache vitendo vibaya, na kuwaondoa watu katika giza na kuwapeleka kwenye nuru.
5. Mitume wanakuja duniani wakati gani?
   Mitume wanakuja duniani wakati ule watu wanapoacha njia ya Mungu na wanapofanya vitendo vibaya, na wakati ule unapodhihirika ufisadi na uovu, uwongo na dhuluma katika dunia.
6. Je, ufisadi na dhuluma na uwongo na vitendo vibaya haya yote yamekwisha duniani?
   La, hayajaisha duniani yataendelea mpaka Siku ya Kiyama.
7. Je, sasa kudhihirika kwa mitume kunaendelea au kumekwisha?
   La, hakuwezi kwisha kwa sababu mambo maovu hayajaisha.
8. Toka mwanzo wa dunia mpaka sasa Mitume wangapi walikuja duniani?
   Mitume wamekuja wengi duniani lakini hakuna anayejua hesabu

yao sawasawa ila Mungu tu.

9. Bainisha majina ya baadhi ya Mitume waliotajwa na Kurani Takatifu.
   Adam, Nuhu, Ibrahim, Yusuf, Daudi. Zakaria, Saleh, Musa, Harun, Yahya, Isa, Muhammad, amani ya Mungu juu yao.
10. Namna ngapi za Mitume?
    i. Kwanza ni Mitume wa sheria yaani Mitume waliokuja na sheria mpya kutoka kwa Mungu, kama Musa na Mtume wetu Muhammad (s.a.w.).
    ii. Pili ni Mitume wasiopewa sheria mpya, kusudi la kufika kwao ni kutangaza sheria ya Mungu aliyopewa Mtume wa kwanza, kama nabii Isa alikuja kutangaza sheria ya nabii Musa na Seyidna Ahmad amefika kutangaza sheria ya Mtume Muhammad, katika siku hizi.
11. Je, Nabii ni mwanadamu?
    Naam, nabii ni mwanadamu.
12. Je, nabii anakula na kunywa maji kama watu wote?
    Naam, nabii anakula na kunywa maji kama watu wote.
13. Je, nabii anakufa?
    Naam, nabii anakufa kama wanavyokufa watu wote.
14. Je, inawezekana kwa nabii au mtu ye yote kupelekwa mbinguni na kiwiliwili chake?
    Haiwezekani kwa nabii au mtu ye yote kupelekwa mbinguni na kiwiliwili chake.
15. Je, nabii hana dhambi kabia?
    Nam, nabii hana dhambi kabisa, na ni mtukufu kabisa.

## SOMO LA TANO
## MTUME MUHAMMAD MTUKUFU s.a.w.

1. Muhammad ni nani?
   Muhammad ni Mtume wa Mungu na Mjumbe wake.
2. Alidhihirikia katika mji gani?
   Alidhihirikia mji wa Makka, bara Arabu.

3. Je, Mtume Muhammad alitumwa kwa Waarabu tu au kwa watu wote?
   Yeye alitumwa kwa watu wote wa duniani na kwa kila kabila na kila nchi, naye alisema: "Mimi ni Mjumbe wa Mungu kwenu wote."
4. Je, Mitume wote waliokuja kabla ya Mtume Muhammad walitumwa kwa dunia yote?
   La, hawakutumwa kwa dunia yote bali kila mtume alitumwa kwa kabila yake tu, kama vile nabii Isa alitumwa kwa Waisraeli tu.
5. Niambie hali ya Mtume Muhammad, amani ya Mungu juu yake, kwa kifupi.
   Mtume Muhammad Mtukufu alizaliwa katika mji wa Makka na jina la baba yake ni Abdullah bin Abdul Muttalib, na jina la mama yake ni Amina. Baba yake alikufa kabla yeye hajazaliwa, na mama yake alikufa Mtume alipokuwa na umri wa miaka sita. Kwa hiyo akawa yatima.
   Baadae alikaa kwa babu yake miaka miwili, lakini pia na babu yake akafa. Wakati ule Waarabu walikuwa wanaabudu masanamu, lakini Mtume Muhammad hata vile umri wake ulikuwa mchache pia alikuwa anakimbia kuabudu masanamu na aliyachukia kabisa. Desturi zake alikuwa anakaa faraghani na kufikiri habari za Mungu. Wala hakuwa mwenye kupoteza wakati wake katika michezo.
   Alipokuwa kijana yaani mtu mzima alimaliza siku zake zote katika kutumikia viumbe, kusaidia maskini, na kutenda vitendo vyema, alikuwa msema kweli na mwaminifu sana. Siku hizo alikuwa mashuhuri sana kwa kusema kweli na uaminifu hata watu walikuwa wakimfanya kama hakimu baina yao.
   Alipenda sana kuabudu Mungu hata alikuwa akienda katika pango linaloitwa Hira na kukaa huko siku nyingi katika kumwabudu Mwenyezi Mungu wake.
   Hata siku moja alipokuwa yumo katika kumwabudu Mola wake akajiwa na Jibril na akaambiwa maneno ya Mungu. Wakati ule umri wake ulikuwa miaka arubaini. Na baada ya kupata utume alikaa Makka miaka kumi na tatu na wakati ule alikuwa anabashiri katika watu wa Makka, wengi wao walikataa na watu kidogo wakamfuata; na waliomkataa wakawa maadui zake, na walikuwa wanampiga na kumtukana yeye pamoja na masahaba wake, hata

akahama Makka kwa amri ya Mungu kwenda Madina pamoja na Sahaba wake. Akakaa miaka kumi. Na katika wakati huo vile vile alibashiri maneno ya Mungu kwa watu wa Madina. Alipata mashaka pamoja na masahaba zake kwa makafiri, na wanafiki, lakini mwishoni makafiri hawakupata makusudi yao, na Mtume alipata kustawi na raha. Watu wengi walikubali na wakaingia katika Dini ya Kiislamu. Akatangaza dini ya Mungu katika Madina na miji mingine. Mwaka wa kumi baada ya kuhama kwake alikwenda Makka pamoja na masahaba zake elfu kumi, na aliingia katika Makka akafuzu.

Maadui zake walichukuliwa mbele yake kwa kutekwa na kufungwa minyororo. Lakini Mtume Muhammad (s.a.w.) aliwasamehe makosa yao na aliwapa uungwana.

Kwa wema aliowatendea maadui zake, wengi wao waliingia katika dini ya Kiislam na wakamsadiki, na baada ya haya kwa wepesi waliingia makabila ya Waarabu katika dini ya Kiislamu. Na ukweli ulidhihirika na uwongo ulivunjika. Ukasimama umoja wa Mungu, kuabudu masanamu kukavunjika.

Alipokuwa na umri wa miaka sitini na tatu akapata ugonjwa, lakini hakuacha kumwabudu Mola wake, hata siku ya Jumatatu tarehe 12 Rabiul-Awwal (mwaka wa 632) akafariki dunia. Sisi tu wa Mungu na kwake tutarejea.

6. Je, Mtume Muhammad alikuwa mtukufu na alikuwa hana dhambi?
   Naam, alikuwa mtukufu kabisa na alikuwa hana dhambi.
7. Je, Mtume Muhammad, amani ya Mungu juu yake ndiye nabii wa mwisho?
   Naam, ndiye nabii wa mwisho wa sheria, maana hatakuja nabii wa sheria mpya baada yake mpaka siku ya Kiyama.
8. Je, inawezekana kuja baada yake nabii asiye na sheria?
   Naam, inawezekana kuja nabii asiye na sheria mpya baada yake.
9. Khatamul-Ambiyai maana yake nini?
   Maana ya Khatamul- Ambiyai ni Mahuri wa Mitume.
10. Mradi gani katika muhuri wa rnitume?
   Kama vile muhuri umewekwa kuisadikisha barua, na hivi Mtume wetu Muhammad, amani ya Mungu juu yake ni muhuri wa mitume, maana ndiye aliyekuja na kusadikisha mitume wote. Na lau kama

yeye hakutuambia na kusadikisha isingewezekana kwetu kusadiki manabii waliopita kwa sababu sisi hatukuona hali yao.

## SOMO LA SITA
## KURANI TAKATIFU

1. Kurani ni nini?
   Kurani ni jina la kitabu cha sheria ya Kiislamu kilichoteremshwa na Mungu.
2. Kurani Takatifu kimeteremshwa juu ya nani?
   Kurani Takatifu kimeteremshwa juu ya bwana wetu Muhammad Mtume wa Mungu.
3. Kurani Takatifu kimeteremshwa katika lugha gani?
   Kurani Takatifu kimeteremshwa katika lugha ya Kiarabu.
4. Kurani Takatifu kimeteremshwa katika lugha ya Kiarabu kwa sababu gani?
   Mwenyezi Mungu ameteremsha Kurani Takatifu katika lugha ya Kiarabu kwa sababu lugha hii ni mama ya lugha zote, na ni bora, na kubwa kuliko zote.
5. Je, kujifunza lugha ya Kiarabu ni lazima?
   Naam, ni lazima maana tukijua lugha ya Kiarabu tutafahamu sheria; na tutakapojua sheria vizuri tutafanya vitendo vizuri.
6. Je, juu ya hayo iko faida nyingine ya kujifunza lugha ya Kiarabu?
   Naam, inapatikana katika lugha hii elimu nyingi sana, kama elimu ya Tarehe ya Kiislamu, na hali ya Mtume Mtakatifu na masahaba zake na wafalme wa Kiislam. Na zaidi ya hayo yule anayejua Kiarabu kila pahali anapokwenda atapata wa kusema naye.
7. Je, inawezekana kufasiri Kurani Takatifu katika lugha zingine?
   Naam, inawezekana kufasiri Kurani Takatifu katika lugha zingine.
8. Je, lazima kusoma Kurani, na kusikiliza?
   Naam, lazima kuisoma Kurani na kuisikiliza siku zote.
9. Faida ya kusoma Kurani ni nini?
   Faida ya kusoma na kufahamu Kurani ni zaidi ya hesabu. Lakini hasa moyo wa mtu unatakasika, na unaingiwa na mapenzi ya Mungu. Na mtu anaposoma Kurani anajua njia ya ukweli na

anaendelea juu yake sawasawa na anapata faida ya uzima, na kusudi la maisha yake. Na anajilinda nafsi yake na vitendo vibaya.

10. Je, vipo vitabu vingine vilivyoteremshwa na Mungu kabla ya Kurani?
    Naam, vipo vitabu vilivyoteremshwa na Mungu kama Zaburi, Taurati na Injili.
11. Je, inawezekana kupatikana faida katika kufuata vitabu hivi kama inavyopatikana faida katika kufuata Kurani?
    Haipatikani faida katika kufuata vitabu hivi kama inavyopatikana faida katika kufuata Kurani.
12. Kwa sababu gani haipatikani faida katika kufuata vitabu hivi?
    Kwa sababu Mwenyezi Mungu amekwisha vunja kufuata sheria ya vitabu hivi.
13. Tofauti gani baina ya Kurani na vitabu hivi?
    Kurani inahifadhiwa wala haijabadilika, toka kuteremshwa kwake mpaka sasa. Lakini vitabu hivi hivihifadhiwi na vimebadilika. Na vitabu hivi sasa havimo katika lugha viliyoteremshiwa na maneno yake siyo ya asili yaliyoteremshwa na Mungu.
14. Je, baada ya Kurani inawezekana kuteremshwa kitabu kingine chenye sheria mpya?
    La, haiwezekani kuteremshwa kitabu kingine chenye sheria mpya baada ya Kurani.
15. Je, inawezekana kuja nabii na kitabu cha sheria mpya baada ya Kurani?
    La, haiwezekani kuja nabii na kitabu cha sheria mpya baada ya Kurani, lakini bila ya kitabu cha sheria mpya inawezekana kuja nabii.
16. Siku hizi anayefahamu Kurani vizuri ni nani?
    Siku hizi wanaofahamu Kurani vizuri ni Seyidna Ahmad, Mjumbe wa Mungu, na wafuasi wake yaani Jamaa Ahmadiyya.

# SOMO LA SABA
# SUNNA NA HADITHI

1. Njia ngapi za kuongoza?
   Njia za kuongoza ni tatu:-
   i. Kurani Takatifu.
   ii. Sunna.
   iii. Hadithi.
2. Maana ya Sunna ni nini?
   Maana ya sunna ni desturi, lakini neno hili linapotumika katika Kiislamu mradi wake ni desturi za Mtume Muhammad Mtakatifu.
3. Mradi gani katika desturi za Mtume?
   Mradi wake ni vitendo vya Mtume alivyofanya zama za uhai wake kwa kuzifuatia amri za Kurani.
4. Faida ya Sunna ni nini?
   Tunajua njia ya kufanya vitendo vingi vya sheria ya Kiislamu na njia ya kusali na kutawadha na njia ya kufunga saumu na vinginevyo, kwa sababu ya Sunna.
5. Vifungu vya Sunna ni vingapi?
   Vifungu vya Sunna ni viwili:-
   Fungu la kwanza ni la lazima, kama rakaa mbili za sunna ya sala ya asubuhi na sunna za sala zingine.
   Fungu la pili si la lazima kama kufunga saumu ya siku sita za Shawwal.
6. Je, kufuata sunna ni lazima?
   Kufuata Sunna za fungu la kwanza ni lazima, na kufuata Sunna za fungu la pili si lazima, lakini kama mtu akifuata ni vizuri sana.
7. Hadithi ni nini?
   Maana ya Hadithi ni maneno, lakini tamko hili katika Kiislamu hutumika hasa kwa maneno ya Mtume Muhammad Mtukufu.
8. Hadithi zimekusanywa lini, na zimeandikwa katika vitabu lini?
   Zimeanza kukusanywa hata katika siku za Mtume na zimeandikwa vitabuni baada ya kupita miaka 100 kufariki kwake Mtume Muhammad (s.a.w.).
9. Tunawezaje kutambua Hadithi za kweli na zisizo za kweli?
   Hadithi inayokuwa sawa na maneno ya Kurani itakuwa ni sahihi

na Hadithi isiyo sawa na maneno ya Kurani itakuwa uwongo, maana Mtume Mtukufu s.a.w. hawezi kusema kinyume cha Kurani.

10. Vitabu vya Hadithi ni vingapi?

    Vitabu vya Hadithi ni vingi sana lakini vitabu vya Hadithi vilivyo mashuhuri ni sita:

    i. Sahihil-Bukhari, kimekususanywa na Imam Muhammad bin Ismail Bukhari Imam huyu aliza-liwa miaka 194 AH. Na kitabu chake husifiwa sana na husomwa sana.
    ii. Kitabu cha Muslim kimekusanywa na Imam Muslim bin Hajjaj na kitabu hiki husomwa sana.
    iii. Sunani-Abi-Daud, kimekusanywa na Imam Abu Daud.
    iv. Jamiu-Tirmidhi, kimekusanywa na Imam Tirmidhi.
    v. Sunani-Nasai, kimekusanywa na Imam Nasai..
    vi. Sunani-Ibn-Majah, kimekusanywa na Ibn Majah.

# SOMO LA NANE
# DHAMBI

1. Dhambi ni nini?

   Dhambi ni kitendo kiletacho ugonjwa rohoni, na kwa sababu ya kitendo hicho Mungu anakasirika. Kwa kifupi kumwasi Mwenyezi Mungu ni dhambi.

2. Dhambi ni namna ngapi?

   Dhambi ni namna tatu:-

   i. Ya kwanza ni dhambi ya roho.
   ii. Ya pili ni dhambi ya ulimi.
   iii. Ya tatu ni dhambi ya viungo.

3. Kwa nini mtu anafanya dhambi?

   i. Mtu anafanya dhambi, kwa sababu ya ujinga wake, maana hajui mambo gani ni mazuri na mambo gani ni mabaya.
   ii. Na kwa sababu ya urafiki wa watu wabaya. Kila mtu anataka kufuata desturi ya rafiki yake. Na ikiwa rafiki yake ni mtu mbaya nae pia atakuwa mtu mbaya.
   iii. Kwa sababu ya desturi au ada, maana watu wanajua kwamba uwongo ni dhambi na mwisho wake ni adhabu.

Lakini baada ya kujua ubaya wa uwongo wanasema uwongo, kwa sababu ni desturi yao kusema uwongo.

4. Mtu anawezaje kujiepusha na dhambi?
   Mtu anaweza kujiepusha na dhambi kwa kuondoa ujinga wake na kujifunza elimu ya Dini. Na asifanye urafiki na watu wabaya, wala asifuate vitendo vyao vibaya. Na aache desturi zake mbaya.
5. Mtu anawezaje kuacha dhambi akipata elimu?
   Dhambi ni kama sumu, na mtu anapojua kuwa katika maziwa haya mna sumu, na inaua, yeye hawezi kunywa maziwa haya, na vile vile mtu anapojua kuwa dhambi inatupa mtu katika adhabu hawezi tena kufanya dhambi.
6. Niambie baadhi ya madhambi.
   Madhambi ni namna nyingi, lakini sasa nitakuambia baadhi ya madhambi. Kusema uwongo, kula mali ya watu bila haki, bughudha, kiburi, dhuluma, kusengenya, kudanganya, kuua, kwiba, kupigana, kuzini, kutukana, riba, rushwa, kumshiriki Mungu, kukufuru yaani kukataa Mungu na Mtume wake na vitabu vyake. Na kutumia kila kitu kilichoharimishwa na Mwenyezi Mungu na Mtume wake.
7. Vitu gani vilivyoharimishwa na Mwenyezi Mungu?
   Kufanya pombe, kuuza pombe, na kunywa pombe, kucheza kamari, kula nyama ya nguruwe na mnyama asiyechinjwa kwa jina la Mungu, damu, wanyama waliokufa, mnyama aliyekufa kwa kuanguka, mnyama aliyekufa kwa kupigwa, wanyama wakali wenye kucha kama simba, mbwa wa mwitu na vinginevyo.
8. Katika nchi hii baadhi ya watu wanapochinja mnyama wanakata shingo yake yote mara moja, Je, njia hii ni sawa?
   Njia hii si sawa. Njia ya kweli ni kuchinja mnyama wala isikatwe shingo yake yote mara moja, baada ya kuchinja lazima kungojea mpaka damu yote itoke na mnyama afe, baadaye unaweza kukata shingo yote.
9. Mtu mwenye dhambi atafanyaje ili kusamehewa?
   Juu yake kujuta na kuomba msamaha kwa Mwenyezi Mungu na kuahidi kuwa hatafanya tena dhambi kabisa na baada ya haya afanye vitendo vyema atasamehewa.

10. Nani asiyesamehewa?
    Ni yule anayefanya dhambi na kutubia halafu arudie tena kufanya dhambi wala asifanye vitendo vyema.
11. Je, inawezekana kuadhibiwa mtu mwema badala ya mtu mwenye dhambi?
    La, haiwezekani kuadhibiwa mtu mwema badala ya mtu mwenye dhambi.
12. Je, mtu akiona mtu anafanya dhambi afanyeje?
    Juu yake kama anaweza kumkataza amkataze kwa viungo vyake au amkataze kwa ulimi wake, na kama hawezi basi achukie na amwombee kuwa Mungu amsuluhishe.

## SOMO LA TISA
## WEMA

1. Wema ni nini?
   Wema ni vitendo vilivyo vizuri vinavyofanywa kwa kupata amri za Mungu. Kwa kifupi kumtii Mwenyezi Mungu ni wema.
2. Wema ni namna ngapi?
   Wema ni namna tatu:-
   i. Ya kwanza, wema wa roho yaani yenye kufikiri mema.
   ii. Ya pili wema wa ulimi, yaani ulimi wenye kusema maneno mema.
   iii. Ya tatu, wema wa viungo, yaani mtu kufanya wema na viungo vyake.
3. Faida ya wema ni nini?
   Mtu mwenye kufanya wema anapata faida nyingi:-
   i. Ya kwanza, anapata mapenzi ya Mungu na hii ndiyo faida kubwa.
   ii. Ya pili, watu wanamtazama kwa heshima na kumtukuza. Na kila mtu anapenda kukaa pamoja naye.
   iii. Ya tatu, wema unamwondolea makosa.
4. Mtu anawezaje kufanya wema?
   Anaetaka kupata uwezo wa kufanya wema, lazima apate elimu ili

ajue jambo gani la wema. Na kukaa katika kikao cha watu wema, na kusikiliza na kufuata maneno yao.

5. Vitendo gani vya wema?

   Vitendo vya wema ni vingi kama kumkumbuka Mwenyezi Mungu, kufuata sheria, kutangaza Dini, Kuvunja dini ya uwongo kwa dalili, tohara yaani kusafisha kiwiliwili na nguo, usawa yaani kuhukumu sawasawa, kutoa sadaka hasa kwa kuwafaa maskini, uaminifu, msamaha, ukarimu. kusaidia, kupatanisha, kutimiza miadi. kukaribisha kwa furaha, kusitiri aibu za watu, kuheshimu watu, kukaribisha wageni kwa heshima, kuwatumikia watu, kufundisha elimu, kulinda heshima ya Jamaa na Dini, ushujaa, kujifunza elimu, kushukuru, kufanya wema kwa kudumu, subira, kutafuta ukweli, kukubali ukweli, kutii wazazi, (lakini wakisema neno kinyume na dini hawafuatwi); kufanya wema kwa wanyama, huruma.

6. Je, yule asiyefanya dhambi wala wema ni mtu mwema?

   Mtu mwema ni yule anayefanya wema haiwezekani mtu kuwa mwema mpaka afanye wema.

## SOMO LA KUMI
## SALA

1. Sala ni nini?

   Sala ni nguzo ya pili ya Kiislamu na maana ya sala ni dua au kuomba kwa Mwenyezi Mungu.

2. Sharti za sala ni ngapi?

   Sharti za sala ni sita:-

   i. Mwili uwe safi na nguo za mwenye kusali ziwe safi.
   ii. Pahali pa kusalia pawe safi.
   iii. Uso uelekee upande wa Kibla.
   iv. Kunuia kwa sala.
   v. Uchi uwe umefunikwa (mtu avae vizuri).
   vi. Iwe wakati wa Sala

3. Sala za faradhi ni ngapi kwa Waislam?

   Sala za faradhi ni tano kwa Waislam:-

i. Sala ya Adhuhuri.
ii. Sala ya Alasiri.
iii. Sala ya Magharibi.
iv. Sala ya Isha.
v. Sala ya Alfajiri.

4. Sala hizi zinasaliwa wakati gani na rakaa za kila sala ni ngapi? :-
   i. Sala ya Adhuhuri, mwanzo wa kuteremka jua mpaka saa tisa. Rakaa nne zilizo sunna na nne zilizo faradhi na rakaa mbili za sunna baada ya faradhi.
   ii. Sala ya Alasiri tangu saa tisa mpaka jua kuchwa. Rakaa nne zilizo faradhi.
   iii. Sala ya Magharibi, tangu kuchwa jua mpaka kupotea mawingu mekundu, rakaa tatu zilizo faradhi na mbili za sunna.
   iv. Sala ya Isha, tangu kupotea mawingu mekundu mpaka nusu ya usiku. Rakaa nne zilizo faradhi na mbili za sunna na tatu za Witri.
   v. Sala ya Asubuhi inasaliwa toka mwanzo wa Alfajiri mpaka kutoka jua. Ina rakaa mbili zilizo sunna, na mbili zilizo faradhi.
5. Faida ya sala ni nini?
   Faida ya kwanza ya sala alivyosema Mungu ni:
   "Hakika sala inazuia mambo ya aibu na ushupavu na uasi" (Kurani).
   Faida Ya pili, moyo wa mtu unakuwa safi na yanaingia rohoni mapenzi ya Mwenyezi Mungu.
6. Je, Sala ya safari na sala ya mkazi wa mjini ni sawa?
   Si sawa. Katika safari Sunna hazisaliwi ila sunna ya Asubuhi. Na sala za faradhi zinasaliwa nusu ya sala ya mkazi wa mji, ila sala Asubuhi na sala ya Magharibi.
7. Sala ya jamaa na sala ya mmoja ipi bora?
   Sala ya jamaa ni bora kuliko sala ya mmoja.
8. Je, sala ni faradhi juu ya wanawake?
   Naam, sala ni faradhi juu ya wanawake; lakini katika hali ya hedhi, na katika damu ya nifasi (damu ya kuzaa) sala imekatazwa kwa wanawake.
9. Je, sala ni lazima juu ya watoto?
   Sala ni lazima juu ya watoto wanapopata umri wa miaka kumi na mbili. Na lazima kwa wazee kuwafundisha watoto wao kabla ya

umri huo.

10. Mwenye kuacha sala hukumu yake ni nini?
    Anasema Mtume Mtakatifu: mwenye kuacha sala kwa kusudi, hakusahau, amekwisha kukufuru.
11. Seyidna Ahmad amesema nini juu ya sala?
    Amesema: "Simamisheni sala zenu tano kwa unyenyekevu na upole wa moyo kama yule mwenye kumwona Mungu."

## SOMO LA KUMI NA MOJA
## KUFUNGA SAUMU YA RAMADHANI

1. Kufunga Saumu ni nini?
   Kufunga Saumu ni nguzo ya nne ya Kiislamu na hakika ya Kufunga ni kuacha kula na kunywa toka asubuhi mpaka magharibi kama Mugu alivyoamrisha. Na kuacha kila mambo mabaya.
2. Saumu ya faradhi ni katika mwezi gani?
   Saumu ya faradhi ni katika mwezi kamili wa Ramadhani.
3. Kufunga saumu ya Ramadhani ni lazima juu ya nani?
   Kufunga saumu ya Ramadhani ni lazima juu ya kila Mwislam isipokuwa watoto wadogo, wagonjwa, wadhaifu sana, wenye mimba, wanyonyeshao na wasafiri.
4. Mwenye kuacha kufunga saumu ya Ramadhani kwa kusudi bila udhuru wo wote, hukumu yake ni nini?
   Mwenye kuacha kufunga saumu ya Ramadhani bila udhuru wo wote anapata dhambi kubwa na mwenye kufunga kisha akafungua bila sababu basi juu yake afunge siku sitini kwa mfululizo, au alishe maskini sitini.
5. Je, kufunga katika mwezi mwingine ni faradhi?
   Kufunga katika mwezi mwingine si faradhi, Lakini mtu akifunga anapata thawabu na kama hakufunga hana dhambi.
6. Kufunga saumu kumekatazwa katika siku gani?
   Kufunga saumu kumekatazwa siku za idi mbili, ndogo na kubwa, na pia kufunga siku ya ljumaa peke yake tu, imekatazwa. Na kama mtu anataka kufunga siku ya Ijumaa, basi na aanze siku ya Alhamisi

halafu Ijumaa, au siku ya Ijumaa pamoja na Jumamosi, lakini kufunga siku ya Ijumaa peke yake imekatazwa.

7. Mwenye kufunga kama hakuacha vitendo vibaya au maneno mabaya saumu yake ni kamili?
   La, saumu yake si kamili wala hapana faida katika kufunga saumu ya namna hii; mradi wa kufunga hasa ni kuacha vitendo vibaya na maneno mabaya.
8. Wakati wa kula daku na wakati wa kufuturu ni upi?
   Wakati wa kula daku ni kabla ya kutoka alfajiri, yaani karibu ya saa kumi mpaka kutoka alfajiri. Na wakati wa kufuturu ni pale jua linapokuchwa. Lazima kufuturu mara moja wala usingojee-ngojee.
9. Saumu inaharibikaje?
   Saumu inaharibika kwa kula na kunywa kwa kusudi, na kwa kuja damu ya hedhi, na kwa kuingiliana mwanamume na mwanamke.
10. Je, inavunjika saumu kwa kupiga miswaki na kuoga na kujipaka mafuta katika hali ya kufunga?
    La, haivunjiki saumu kwa kutumia vitu hivi katika hali ya kufunga saumu.
11. Faida ya kufunga saumu ni nini?
    Kufunga saumu kunamletea mtu kuwa na subira na kuweza kukataza nafsi yake katika maasi na madhambi. Na vile vile kufunga kunatakasa moyo wa mtu, na kunafanya roho ya mtu kupenda kutenda vitendo vyema. Na faida kubwa ni kama alivyosema Mwenyezi Mungu, "Nami ni malipo ya kufunga," yaani mwenye kufunga kwa nia safi kama Mungu alivyoamrisha atampata Mungu, yaani atakutana na Mungu.
12. Seyidna Ahmad alisemaje juu ya kufunga saumu?
    Alisema, "Timizeni saumu yenu kwa ukweli na nia safi,"

# SOMO LA KUMI NA MBILI
# KUTOA ZAKA

1. Zaka ni nini?
   Zaka ni nguzo ya tatu ya dini ya Kiislamu, na tendo la faradhi. Maana ya Zakat ni kutakasa, au kuzidisha. Na mali ile inayotolewa, kwa nia ya kutimiza faradhi hii, vile vile huitwa zakat.
2. Kutoa zaka ni faradhi juu ya nani?
   Kutoa zaka ni faradhi kwa mtu mwenye nisabu kamili iliyopitiwa mwaka mzima.
3. Nisabu ni nini?
   Nisabu ni kadiri ya mali awezayo kutoa zaka. Na nisabu ya kila kitu ni mbalimbali.
4. Juu ya vitu gani inawajibika kutoa zaka?
   Inawajibika kutoa zake juu ya fedha, dhahabu, sarafu, ngamia, ng'ombe, mbuzi, kondoo, zabibu, na vitu vya biashara.
5. Katika mwaka mmoja zaka hutolewa mara ngapi?
   Katika mwaka mmoja zaka hutolewa mara moja.
6. Bainisha sehemu ya zaka inayotolewa katika Nisabu.
   Sehemu ya zaka inayotolewa katika Nisabu ni sehemu moja kwa kila sehemu arobaini (1/40).
7. Je, kila mtu ana hiyari kugawa mali ya zaka kama anavyotaka?
   La, hapana ruhusa kwa mtu kugawa zaka kama anavyotaka. Lakini atoe kwa Imam, na Imam atagawanya kama alivyoamirisha Mungu.
8. Mali ya zaka inagawanywa kwa nani?
   Mali ya zaka hupewa maskini na mafukara na wasafiri, na hao wanaokusanya mali ya zaka na kukomboa mateka na kulipa katika njia ya Mungu na kueneza Uislam.
9. Faida ya kutoa zaka ni nini?
   Faida ya kwanza ya kutoa zaka ni kuwa hao tuliowataja kama watapata mali ya zaka wataishi kwa raha. Faida ya pili ni kuondoa umaskini.
10. Seyidna Ahmad alifundishaje juu ya kutoa zaka?
    Alifundisha hivi: "Kila mwenye kuwa na faradhi ya kutoa zaka basi na atoe."

# SOMO LA KUMI NA TATU
# KUHIJI

1. Kuhiji ni nini?
   Kuhiji ni nguzo ya tano ya dini ya Kiislamu. Na kuhiji ni ibada inayoabudiwa katika Makka.
2. Kuhiji ni lazima juu ya nani?
   Kuhiji ni lazima juu ya Mwislamu mwenye mali ya kutosha safari yake kwenda Makka na kurudi, na pia aache kwa watoto wake mali ya kuwatosha kwa mahitaji yao, na pia lazima njia ziwe hazina hatari.
3. Kuhiji ni katika miezi gani?
   Kuhiji ni katika miezi ya Shawwal, na Dhulqaada na siku kumi za kwanza za Dhulhiji.
4. Wakati wa Kuhiji nguo gani inayokatazwa kuvaliwa?
   Wakati wa kuhiji hapana ruhusa. kuvaa shati au kanzu wala kilemba wala suruali wala kofia.
5. Nguo gani inayovaliwa wakati wa kuhiji?
   Wakati wa kuhiji huvaliwa shuka kiunoni na shuka nyingine ya kujitanda.
6. Kitendo gani cha mwisho wa kuhiji?
   Kitendo cha mwisho wa kuhiji ni kuchinja wanyama siku ya kumi ya mwezi wa Dhulhiji na baadaye kunyoa na kuzunguka Kaaba mara saba.
7. Je, inawezekana mtu kuhiji badala ya mwenye faradhi ya kuhiji?
   Naam inawezekana mtu mwingine kuhiji badala ya mtu mwenye faradhi ya kuhiji.
8. Kuhiji kunadhihirisha nini?
   Kuhiji kunadhihirisha kuwa mpenzi wa Mungu, hawezi kupata utulivu wa roho katika mambo ya dunia bali anapata utulivu wa roho katika kujitupa kwa Mungu yeye na mali yake.
9. Faida ya kuhiji ni nini?
   Mtume mtakatifu amesema kuwa: Mwenye kuhiji kwa nia safi na vitendo vyema atakuwa kama siku ile aliyozaliwa na mama yake, yaani atakuwa mtukufu.

10. Seyidna Ahmad a.s. alifundishaje juu ya habari ya kuhiji?
Seyidna Ahmad a.s. alifundisha kama alivyofundisha Mtume Mtakatifu Muhammad (amani na rehema za Mungu ziwe kwake). Na ameandika, "Mwenye faradhi yake kuhiji na hapana kitu chenye kumzuia basi ahiji kwenye nyumba ya Mungu-Kaaba:"

# SOMO LA KUMI NA NNE
# SEYIDNA AHMAD a.s., MASIHI ALIYEAHIDIWA

1. Unapozidi ufisadi na mambo maovu Mungu hufanyaje?
Wakati wa namna hiyo Mungu hutuma mjumbe wake kuondoa ufisadi na mambo maovu.
2. Je, siku hizi ufisadi na mambo maovu yanaonekana?
Naam, yanaonekana. Na watu wa dunia wamemsahau Mungu na wanashughulika katika mambo maovu.
3. Je, siku hizi Mungu ametuma mjumbe wake kuondoa haya kama ilivyo desturi yake?
Naam' Mwenyezi Mungu ametuma mjumbe wake siku hizi kama ilivyo desturi yake kuondoa ufisadi na uovu.
4. Jina la mjumbe huyo ni nani, na amedhihiri katika mji gani?
Jina la mjumbe huyo ni Hazrat Mirza Ghulam Ahmad a.s. na alidhihirika katika mji wa Kadian bara Hindi.
5. Ikiwa dini ya Kiislam ni kamili basi haja gani tena kutumwa mjumbe mwingine baada ya Mtume Muhammad, amani ya Mungu juu yake?
Mitume hawaji duniani kukamilisha dini tu, bali wanakuja kuondoa ufisadi na uovu na kuwasuluhisha watu na kuwakumbusha amri za Mwenyezi Mungu. Na baada ya Mtume Muhammad, amani ya Mungu juu yake, watu wameacha kufuata amri za Mungu na wameshughulika katika ufisadi na mambo mabaya. Kwa sababu hii Mwenyezi Mungu amemtuma mjumbe baada ya Mtume Mtakatifu Muhammad; na mjumbe huyo ndie Imam Mahdi aliyekuja ili kukumbusha amri za Mungu na kuwasuluhisha watu.

6, Je, inawezekana kuja mjumbe mwingine kama huyu baada ya Mtume?
Naam, inawezekana kuja mjumbe mwinge ili kuwasuluhisha watu na kusimamisha sheria ya Kiislam baada ya Mtume Muhammad Mtakatifu, lakini lazima awe chini ya Mtume Muhammad (s.a.w.).

7. Je, Seyidna Ahmad ni mjumbe wa namna hii au namna nyingne?
Seyidna Ahmad ni mjumbe wa namna hii, yaani Mungu alimtuma Seyidna Ahmad ili asimamishe sheria ya Kiislam na kuondoa ufisadi na kuwasuluhisha watu.

8. Je, kumfuata Seyidna Ahmad mjumbe wa siku hizi ni lazima?
Naam, Kumfuata yeye ni lazima kwa sababu yeye ni mjumbe wa Mungu, na kumfuata mjumbe wa Mungu ni lazima juu ya kila mtu.

9. Watu wanaomfuata Syidna Ahmad, mjumbe wa siku hizi, wanaitwaje?
Watu wenye kumfuata wanaitwa Waislamu Waahmadiyya.

10. Je, alipata kutunga kitabu cho chote Seyidna Ahmad?
Naam, alitunga vitabu zadi ya 80 kwa Kiarabu na Kiurdu na akaeleza humo ubora wa Uislamu na maelezo ya Kurani.

## SOMO LA KUMI NA TANO
## SIKU YA KIYAMA

1. Kiyama ni nini?
Watu wote watakapokufa na vitu vitangamizwa na hakitabaki cho chote duniani Mungu atawafufua watu wote na wataulizwa vitendo vyao walivyotenda duniani na kila mtu atapewa ujira sawa na alivyotenda. Basi hii ni Kiyama na vile vile huitwa Akhera.

2. Saa Ya Kiyama itakuwa lini?
Hapana anayejua saa ya Kiyama itakuwa lini ila Mwenyezi Mungu tu.

3. Alama za Kiyama ni zipi?
Alama za saa ya Kiyama ni nyingi sana, lakini zinazojulikana ni hizi:-

i. Watu wataacha kufuata Sheria, na watashughulika katika mambo maovu.
ii. Fitina na Machafuko yatakuwapo.
iii. Watu wasio na sifa njema watapewa cheo kikubwa
iv. Watu watakula mali ya haramu.
v. Ataonekana Addajjal: atakuwa hana jicho la kulia, yaani hatakuwa na dini sawasawa. Na atakuwa adui wa Uislam.
vi. Ataonekana Masihi aliyeahidiwa, yaani si Masihi mtoto wa Mariam bali atakuja mtu mwingine kama yeye katika Umati wa Mtume Muhammad, (amani ya Mungu juu yake), na atavunja msalaba kwa dalili na ataua nguruwe, yaani atabadilisha tabia ya watu waliokuwa na tabia kama ya nguruwe, na atasimamisha haki na atahukumu kwa adili baina ya hitilafu za watu.

4. Je alama hizi za saa ya siku ya Kiyama zimekwisha dhihirika?
   Naam, zimekwisha dhihirika. Na amekwisha dhihirika siku hizi Masihi na Mahdi aliyeahidiwa. Naye ni Seyidna Hadhrat Mirza Ghulam Ahmad, katika mji wa Kadian bara Hindi.
5. Itakuwa nini siku ya Kiyama?
   Atahesabiwa kila mtu na wale wenye vitendo vyema wataingia katika Janna. Na wenye vitendo vibaya wataadhibiwa na watatupwa katika Jehanam.
6. Janna ni nini?
   Janna ni pahali pa thawabu na neema, na ndani yake zimo daraja mbali mbali na hao wanaoingia katika Janna (Peponi hawatatoka watakaa humo milele.
7. Jehanam ni nini?
   Jehanam ni pahali pa adhabu. Na ndani yake mna daraja mbali mbali. Na wanaoingia katika Jehanam (Motoni) mwishoni watatolewa.

# SOMO LA KUMI NA SITA
# JIHADI

1. Jihad! ni nini?
   Jihadi ni kujitahidi kutangaza Dini ya Mungu na kujitahidi kusimamisha hukumu za Mungu duniani kama alivyoamrisha Mwenyezi Mungu.
2. Je, mtu akisema kuwa "Jihadi ni kupigana na wasioamini, kwa upanga, ili kuwasilimisha au kuwatisha au kuwaangamiza wasipokubali Dini ya Kiislam ni kweli?
   Anayefahamu ya kwamba maana ya Jihadi ni kupigana kwa upanga na makafiri kwa kuwasilimisha watu katika dini basi yeye hakufahamu hakika ya Jihadi. Bali amesema kinyume na sheria ya Kiislamu.
3. Je, Waislam wamepewa amri na Kurani kueneza na kutangaza Uislam kwa upanga?
   La, hawakuamrishwa katika Kurani kutangaza Uislam kwa upanga, wala hawakuamrishwa kupigana na wasioamini, ili kuwasilimisha.
4. Je, Mtume Muhammad, amani Ya Mungu juu yake, ameamrisha kuzagaza Uislamu kwa upanga?
   La, Mtume Muhammad, amani ya Mungu juu yake, hakuamrisha hivi.
5. Je, Uislam umezagaa duniani kwa nguvu ya upanga?
   La, Uislam haukuzagaa kwa nguvu ya upanga. Bali umezagaa kwa mafundisho yake mema na kwa nguvu za dalili na kwa ishara zinazoonyeshwa na Mungu mpaka sasa.
6. Je, Mtume Mtukufu alipigana na makafiri lini na kwa nini?
   Naam, Mtume Mtukufu alipata kupigana na makafri baada ya kupita miaka kumi na mitatu toka kudai kwake kuwa ni Nabii. Kwa sababu makafri walimwondoa katika nyumba yake pamoja na wafuasi wake na walishambulia kwa silaha ili kuwaua na kuwaangamiza na mashambulio ya makafiri yakaendelea siku nyingi, lakini Mtume alisubiri na kuwasubirisha wafuasi wake, hata wakawa katika dhiki kubwa na msiba na mashaka na wakakatazwa kula na kunywa na kutembea kwa uungwana na raha. Basi wakati huo walipewa idhini na Mwenyezi Mungu

kupigana kujikinga na makafiri ili walinde mali zao na jamaa zao, na wake zao, Lakini hawakuweza kuthubutisha kama Mtume Mtukutu na wafuasi wake walichukua silaha kwa sababu ya kupigana na makafiri ili kuzagaza Uislam.

7. Kwa dalili gani unasema kuwa Uislam haukuzagazwa kwa silaha? Nasema kuwa, Uislam haukuzagazwa kwa Silaha, kwa sababu sheria ya Kiislam haifundishi kuzagaza Uislam kwa silaha.
    i. Mungu anasema katika Kurani, "La ikraaha fiddini" yaani hapana ruhusa kuingiza mtu katika dini kwa nguvu. Na vile vile anasema, "Iteni watu kwenye njia ya Mwenyezi Mungu kwa hekima, na maneno mazuri na mawaidha mema. Hii ni amri ya Mungu kwa kuzagaza dini ya Kiislam.
    ii. Lau kama Uislam umezagaa kwa silaha, basi ungezagaa sana wakati ule wa vita. Lakini anayejua hali ya vita na Tarehe ya Kiislam anajua sana kuwa watu hawakuingia wengi katika Uislam wakati wa vita, bali waliingia wakati wa amani walipofikiri na walipofahamu mafundisho ya Kiislam.
    iii. Mwenye kukubali dini kwa karaha au nguvu na shuruti, hawezi kufuata sawasawa, wala hawezi kutoa nafsi yake na mali yake kwenye dini. Lakini kila mtu anajua kuwa wafuasi wa dini ya Kiislam, siku zile walitoa mali zao na roho zao, na wakaacha makazi yao na jamaa zao, na walipata kila msiba na dhiki, lakini hawakuacha dini yao, kwa hivi inadhihirika wazi wazi kuwa hawakuingia kwa karaha au kwa nguvu ya silaha. Lau kama wao waliingizwa kwa karaha wasingeonekana hivi kufuata sawasawa na kutoa kila kitu.
    iv. Sisi tunaona Uislam katika nchi ya Sumatra na Java, na Ulaya na China na Africa na America na pahali penginepo.
    Je, watu wa nchi hizi zote waliingia katika dini ya Kiislam kwa karaha?
    Na nani aliyekwenda katika nchi hizi zote na kupigana vita? Kila mtu anajua kuwa watu wa nchi hizi zote waliingia katika dini ya Kiislam bila karaha wala kupigana vita, bali ni kwa mafundisho mema ya Kiislam, Hivi hivi na watu wa bara Arabu waliingia katika dini ya Kiislam kwa hiari yao. Hakika ubora wa mafundisho ya Kiislam uliwavuta Waislam.

# SOMO LA KUMI NA SABA
# NDOA (NIKAH)

1. Nikah (ndoa) ni nini-
   Maana ya Nikah ni kufungamana. Mwanamume na mwanamke wanapofungamana na kuoana kwa agano kama ilivyo hukumu ya sheria, mafungamano haya huitwa Nikah.
2. Je, Ndoa ni lazima?
   Naam, ndoa ni lazima kwa kila mtu mwenye uwezo na asiyeoa anaasi amri ya Mungu, na anavunja desturi ya Mtume Mtukufu, Mtume Mtukufu amesema 'kuoa ndio desturi yangu, asiyeoa siye wa kwangu.
3. Faida ya kuoa ni nini?
   Kwa kuoa mtu anaweza kuepukana na madhambi mengi kama kutazama wanawake na kuzini na magonjwa mabaya. Na mtu anaweza kuishi kwa utulivu wa moyo. Na vile vile anapata jamaa wengi na ukoo unazidi.
4. Mwanamke gani anayefaa kuolewa?
   Mwanamke anayefaa kuolewa ni yule mwenye dini, mwema na yule mwenye sifa njema na tabia nzuri.
5. Sharti za kuoa ni ngapi?
   Sharti za kuoa ni nne:-
   i. Ya kwanza ni kuulizwa mwanamume na mwanamke kama wanakubali kuoana, kama wanakubaliana waoane, na kama mmoja wao hakukubali, wasioane.
   ii. Ya pili awepo mlinzi, au walii wa yule mwanamke katika jamaa zake, baba yake au ndugu zake na aulizwe kama amekubali kumwoza dada yake au binti yake. Kwani hapana ruhusa mwanamke kuolewa bila ruhusa ya mlinzi wake.
   iii. Ya tatu lazima yawepo mahari. Lakini hapana kiasi maalumu cha mahari. Kila mtu lazima atoe kama anavyoweza sawa na heshima ya mwanamke. Ni lazima kiasi cha mahari kiwe kinaridhisha pande zote mbili. Na mtu asiyetoa mahari ni mwenye dhambi. Na mahari ni mali ya mwanamke si mali ya mwingine.
   iv. Ya nne lazima kukubaliana mbele ya watu na kutangaza ndoa.

6. Ipi njia ya kutangaza ndoa?

Njia ya kutangaza ndoa ni kuwa mmojawapo katika wenye elimu atangaze katika mkutano usio mchache kuliko watu wawili. Yaani kwanza anahutubu hotuba ya ndoa kwa maneno haya:-

***"Alhamdu Lillaahi nahmaduhuu wanastainuhuu wanastaghfiruhuu wanuminu bihii wanatawakkalu alaihi wanaudhu billaahi min shuruuri anfusinaa wamin sayyiaati a'malinaa, man yahdihillaahu falaa mudhilla lahuu waman yudhlilhu falaa haadiya lahuu wanash-hadu allaa Ilaaha illa llaahu wa nash hadu anna Muhammadan abduhuu wa rasuuluhu. Bismillahir-Rahmaanir- Rahiim. Yaa ayyuhalladhiina amanut takullaaha haqqa tuqaatihii walaa tamuutunna illaa wa antum muslimun. Yaa ayyuhannasu-ttaquu rabbakumulladhii khalaqakum min nafsin wahidatin wakhalaka minhaa zaujahaa wabaththa minhumaa rijaalan kathiiran wa nisaa; wattaqu llaahalladhi tasaa'aluuna bihii wal arhaam innallaha kaana alaikum raqiiba. ( 4:1) Yaa ayyuhalladhiina aamanuttaqullaha wa quuluu qaulan sadiidan yuslih lakum a'maalakum wa yaghfir lakum dhunuubakum wa man yuti'illaaha wa rasuulahu faqad faaza fauzan adhiima***. (33:70.71).

Na baadae atangaze kuwa mwanamke fulani ataolewa na mwanamume fulani kama wanakubali kuoana. Kama wanakubali basi wanaoana na wanafunga ndoa. Si haja ya mwanamke kuja katika mkutano wa watu ili akuba1i, bali mlinzi wake aonyeshe kukubali kwake.

7. Baada ya kukubaliana inafanywa nini?

Baada ya kukubaliana mwanamume na mwanarnke wanakuwa mume na mke, na mume anaweza kumpeleka rnke nyumbani kwake Na baada ya kuingiliana; mume awakaribishe jamaa zake na wapenzi wake, na masikini, na awalishe chakula. Kitendo hiki huitwa Walima.. Na hii ni Sunna ya Mtume Mtukufu.

8. Faradhi za mume ni zipi?

Mwanamume amepewa fadhila na Mwenyezi Mungu juu ya mwanamke. Na alifanywa kuwa mlinzi wa mke wake. Kwa hivi ni faradhi juu yake kumpa rnke wake vifao, chakula, nguo na pahali

pa kukaa kama anavyoweza wala asimkasirikie bila haki wala asimpige bila sababu bali ni lazima juu yake kumfanyia wema na kukaa naye kwa mapenzi.

9. Faradhi za mke ni zipi?
   Faradhi za mke ni kumtii mume wake na kufuata hukumu zake zote ila hukumu zenye kuhalifu Sheria asifuate, wala asipoteze mali ya mume wake bali aitumie kwa mahitajio hasa wala asimdhiki mume wake na aangalie heshima yake, wala asifuatane na wanaume wengine. Na faradhi yake kubwa ni kulea watoto vyema, na awe sababu ya kumstarehesha mume wake.
10. Wanawake gani walioharimishwa kuolewa?
    Wanawake hawa wameharimishwa kuolewa:-
    (i) Mama; (ii) Mke wa baba; (iii) Bibi; (iv) Shangazi; (v) Dada za mama; (vi) mama wa kambo; (vii) Dada wa kambo; (viii) Mama ya mke; (ix) Mwanamke mwenye mume; (x) Dada; (xi) Binti; (xii) Binti wa ndugu; (xiii) Binti wa dada; (xiv), Binti wa mke aliyemzaa na mume wa kwanza; (xv) shemeji wakati wa uzima wa mke; (xvi) Binti wa ndugu wa mke; (xvii) Mke wa mtoto; (xviii) Mwanamke mshirikina. (xix) Mwanamke mzinifu.
11. Hukumu ya Kiislam ni ipi katika hesabu ya kuoa wanawake?
    Hukumu ya Kiislam inaruhusu kuoa mpaka wake wanne ikiwa mtu ana haja nao sana. Yaani kama mke wake wa kwanza ana ugonjwa mbaya au hazai au haja zingine za hasa.
    Lakini hapana ruhusa kuoa wake zaidi ya wanne kwa wakati mmoja. Na mtu akioa wake zaidi ya mmoja lazima kwake afanye adili baina yao, awape vitu sawasawa na aende kwao sawasawa, wala asifanye tofauti baina yao. Na kama mtu hawezi kufanya adili baina yao, basi asioe zaidi ya mke mmoja.
12. Talaka ni nini na hukumu zake ni zipi?
    Talaka ni kuvunja agano la ndoa kwa njia ya Sheria ya Kiislam. Ikitokea hitilafu baina ya mke na mume na kwa sababu ya hitilafu hii hawawezi kukaa pamoja kama ilivyoamrisha Sheria, au kama mke akifanya kitendo kinyume cha Sheria, au baba na mama wa mume wakimwambia kuwa mwache mke wako; basi katika hali hii inawezekana mume kumwacha mke wake na kumpa talaka. Na njia ya kutoa talaka lazima mume ampe mke wake talaka, baada

ya hedhi, yaani baada ya kupona, wala bado hajamwingilia. Na ampe talaka mara moja kila mwezi kwa muda wa miezi mitatu. Na miezi mitatu inapokwisha basi mwanamke ana ruhusa kuolewa na mwanamume mwingine. Lakini kama mumewe anataka kumrudia anaweza kumrudia baada ya talaka ya kwanza au ya pili, lakini inapotimau talaka ya tatu haiwezekani tena kumrudia na kumwoa.

Na baada ya talaka tatu na mwanamke akiolewa na mwanamume mwingine, halafu mwanamume huyu akifa au akimwacha basi mume wa kwanza anaweza kumwoa mwanamke huyu.

Hata ikiwa talaka ni jaizi lakini kwa Sheria lazima kabla ya kutoa talaka kusuluhisha baina ya mume na mke wake na kuwafahamisha. Na kama mume hataki kufahamu kukaa pamoja na mke kwa amani mume anaweza kumwacha mke wake na kumwachilia kwa wema. Na kama mwanamke hataki kukaa pamoja na mume wake kwa sababu hasa basi vile vile anaweza kuomba talaka kwa mikono ya Hakimu. Na talaka ya namna hii huitwa Khula.

## SOMO LA KUMI NA NANE
## KUZAA

1. Anapozaliwa mtoto inafanywaje?
   Anapozaliwa mtoto inasomwa Adhana katika sikio lake la kuumeni na inasomwa ikamat katika sikio lake la kushoto; kisha analambishwa kitu kitamu, asali au sukari, na kama hakuna kitu kitamu hata maji yanatosha.
2. Je, mtoto anafanyiwa nini tena baada ya haya?
   Baada ya haya zikifika siku saba mtoto ananyolewa nywele na anapewa jina. Nywele zake zinapimwa na fedha sawa na uzito wa nywele kisha fedha ile inatolewa sadaka kwa maskini.
3. Je, pana jambo jingine linalopasa kufanywa baada ya haya?
   Ndio, siku ya saba au baada yake kwa desturi hutolewa sadaka inayoitwa Akika na vile vile mtoto akiwa wa kiume anatahiriwa.
4. Hukumu za sadaka ya Akika ni zipi?

Kama aliyezaliwa ni mtoto mwanamume, watachinjwa mbuzi wawili baada ya siku saba za kuzaliwa mtoto. Na kama ni mtoto mwanamke atachinjwa mbuzi mmoja. Kisha watapewa maskini na pia watu wengine. Hata jamaa na marafiki watapewa sehemu ya nyama.

# SOMO LA KUMI NA TISA
# MAZIKO

1. Je kila mtu atakufa?
   Naam, kila mtu atakufa.
2. Mtu anapokuwa karibu na kufa inafanywa nini pale?
   Mtu anapokaribia kufa asomewa Sura Yasin, na kama yule mwenye kukaribia kufa anaweza kutoa Shahada basi atoe.
3. Mtu anapopata habari kuwa fulani amekufa aseme nini?
   Mtu anaposikia kufa kwa mtu aseme:-
   *Innaa lillaahi wa innaa ilaihi rajiuun* - yaani: Sisi tu wa Mungu nasi kwake tutarejea. Na baadaye anaoshwa maiti.
4. Maiti anaoshwaje?
   Kama maiti ni mwanamume anaoshwa na wanaume, na kama maiti ni mwanamke anaoshwa na wanawake.
   Njia ya kuosha ni hii:-
   Kwanza mkoshaji atawadhe yeye mwenyewe. Baadae amchambishe maiti na kumtawadhisha, lakini asiweke maji katika pua yake na kinywa chake. Baada ya kumtawadhisha, anaoshwa na kwanza upande wa kulia, na kisha anaoshwa upande wa kushoto. Akoshwe mara tatu au mara tano au zaidi  Maji ya kumkoshea yachemshwe pamoja na majani ya mkunazi na yapozwe kwa maji ya baridi. Maji ya kumkoshea mwisho yatiwe karafuu maiti. Kisha anapakwa karafuu maiti mwilini, na sandani pia. Halafu maiti anavishwa sanda. Mkoshaji akisha mkosha maiti yeye mwenyewe naye akoge.
5. Maiti anavikwaje sanda?
   Mwanamume anavishwa kwa nguo tatu, yaani nguo moja ni shuka ya chini na nguo ya pili ni namna ya kanzu, na nguo ya tatu ni shuka ya kumkunjia ndani yake maiti. Na mwanamke anavishwa kwa

nguo tano, yaani shuka ya chmi, na nguo ya namna ya kanzu na shuka ya kafini na shuka ya kichwani na shuka ya kumkunjia ndani yake.

6. Baada ya kukafini maiti anafanywa nini?
   Baada ya kukafiniwa maiti anasaliwa Sala ya maiti. Na baadaye anazikwa katika kaburi.
7. Wanaoshwaje na wanasaliwaje na wanazikwaje watoto wadogo?
   Watoto wanaume na watoto wa kike wanaoshwa kama watu wakubwa na wanakafiniwa kama watu wakubwa; hapana tofauti baina ya wakubwa na wadogo katika jambo hili, ila dua ya kuomba kwa wakubwa na kwa watoto wachanga inakuwa tofauti.
8. Hukumu gani ya kulilia maiti?
   Kulilia maiti kwa sauti kubwa na kusema maneno mabaya na kuchana nguo na kujipiga makofi yote yamekatazwa na Sheria ya Kiislam. Na hitima na kusoma talakini na kumwombea dua maiti kwa kufukiza ubani (kama wafanyavyo baadhi ya wanawake wa nchi hii) si katika sheria. Na zaidi ya hayo kumwomba dua maiti ni kufuru kubwa.
   Mwanamke aliyefiwa na mumewe akae eda miezi mine na siku kumi. Asijipambe wala asitaabishwe na kupewa dhiki nyingi kama wafanyavyo watu wengine. Matumizi ya mwanamke katika siku za eda ni juu ya warithi wa marehemu mumewe. Mwanamke hana ruhusa kumfanyia msiba mtu asiyekuwa mume wake zaidi ya siku tatu.

## SOMO LA ISHIRINI
## MANENO Y A HEKIMA YA MTUME MUHAMMAD S.A.W.

1. Mambo mawili hayakutani na mtu aliyeamini: ubahili na tabia mbaya.
2. Mungu anapenda sana mambo mawili: upole na subira.
3. Cheleeni kutenda ubaya wa namna mbili: kwenda choo njiani na vivulini.

4. Asiyewashukuru watu hamshukuru Mwenyezi Mungu.
5. Mwenye kujifurahia na kumpenda Mungu na Mtume wake, au atakaye kupendwa na Mungu na Mtume wake, basi aseme kweli anayoyazungumza na kurudisha amana endapo ameaminiwa na kumfanyia wema jirani yake.
6. Lau kama Musa na Isa wangekuwa hai wasingalikuwa na njia ila kunifuata.
7. Mwenyezi Mungu ataleta, baada ya kila miaka mia katika wafuasi wangu mtu wa kuitia nguvu dini ya Mungu.
8. Haamini mtu mpaka ampendelee nduguye kama ajipendeleavyo mwenyewe.
9. Mwenye kula kitunguu saumu au kitunguu maji kwa njaa au kwa vingine basi asisogelee msikitini.
10. Akioga mtu siku ya Ijumaa na akafanya tohara anazoziweza na akapaka mafuta au akajipaka manukato kisha akatoka; asiachanishe kati ya uwili wao kisha akasali na akanyamaza anaposoma Imamu, ataghofiriwa dhambi zake toka Ijumaa ile mpaka Ijumaa ya mbele.
11. Mkamilifu wa imani ni yule mwenye tabia njema. Na bora wenu ni wale watendao wema kwa wake zao.
12. Mwanamke anaposali sala zake tano na akaulinda uchi wake na akamtii mume wake ataingia mlango autakao peponi.
13. Tamaa ya dunia ni mama ya uovu.
14. Mtu ye yote aliye huru hakuna ruhusa kumgeuza mtumwa.
15. Kumgeuza mtu aliye huru kuwa mtumwa ni sawasawa na kumwua.
16. Mwenyezi Mungu hatapokea maombi ya mtu amgeuzae mtu huru kuwa mtumwa
17. Kila kitu kina cha kusafishia, na kitakasacho moyo ni kumkumbuka Mwenyezi Mungu.
18. Hakika kuna kipande cha nyama katika mwili wa binadamu, basi kama ni kizuri, mwili mzima unakuwa mzuri, na kama ni kibaya na mwili mzima unakuwa mbaya, na kumbuka, kipande hicho ni moyo.
19. Pepo iko katika nyayo za mama.
20. Mtoto akiwaheshimu wazee kwa sababu ya ukubwa wao, Mungu atamwekea naye wa kumheshimu atakapokuwa na hali ile miakani.
. 21. Mnafiki ni yule akisema hasemi kweli, akitoa miadi haitimizi, na

akiaminiwa haaminiki.

22. Mwislam ni yule ambae kwa ulimi na mikono yake amewanusuru Waislam wenzake na kuwa katika amani, na Muhajir ni yule aliyeacha yale aliyoyakataza Mwenyezi Mungu.
23. Baba hana zawadi njema ya kuwapa wanawe kushinda mafundisho mema.
24. Nyumba njema ya Mwislam ni ile yenye kulea mwana yatima kwa wema.
25. Mkono uliotoa ni bora kuliko uliopokea.
26. Mtumishi akiwa mlinzi wa mali ya bwana wake lazima ayalinde vilivyo.
27. Wape chakula wenye njaa na watazame wagonjwa, na mwachilie mateka kama kafungwa bila ya haki. Msaidie mnyonge akiwa Mwislam au si Mwislam.
28. Afadhali kukaa mtu peke yake kuliko kuwa na rafiki wabaya; na afadhali kuwa na watu wema kuliko kuwa peke yako. Na afadhali sema maneno kwa kutafuta elimu kuliko kukaa kimya; na kimya ni afadhali kuliko maneno machafu.
29. Wasaidie wake waliofiwa na waume zao.
30. Mtu mwema ni yule atendae mema kwa viumbe vya Mungu.
31. Mtu anayesali na kumkumbuka Mwenyezi Mungu amefanana na mtu aliye hai na mtu asiyesali na hakumkumbuki Mwenyezi Mungu amefanana na mtu aliyekufa.
32. Kila jambo la maana lisiloanzwa kwa kumsifu Mwenyezi Mungu linakuwa halina baraka.
33. Anayekwenda msikitini asubuhi na jioni atabarikiwa kwa ukarimu peponi.
34. Mwenyezi Mungu anapendezwa na hao wanaomshukuru baada ya kula na kunywa.
35. Mwanangu, nataka kukufundisha mambo machache.
    Kila siku mkumbuke Mwenyezi Mungu naye atakukumbuka siku zote. Kama utamkumbuka Mwenyezi Mungu utamwona siku zote kuwa Yu msaidizi wako. Ukiomba cho chote kiombe kwa Mwenyezi Mungu. Ukitafuta msaada utafute kwa Mwenyezi Mungu. Jua kwa yakini kwamba kama ulimwengu mzima unataka kukufanyia wema, hawawezi kukufanyia ila Mungu apende; kama

ulimwengu wote umefunga nia ya kukudhuru, hawatafanya hivyo ila Mungu aruhusu. Uwe karibu na Mwenyezi Mungu utamwona siku zote kuwa Yu, msaidizi wako.

Ukiomba cho chote kiombe kwa Mwenyezi Mungu. Ukitafuta msaada utafute kwa Mwenyezi Mungu. Jua kwa yakini kwamba kama ulimwengu mzima unataka kukufanyia wema, hawawezi kukufanyia ila Mungu apende; kama ulimwengu wote umefunga nia ya kukudhuru, hawatafanya hivyo ila Mungu aruhusu. Uwe karibu na Mwenyezi Mungu katika siku zako za ustawi, ili akukumbuke katika siku zako za shida.

Jua ya kwamba msiba unaoletwa na Mwenyezi Mungu hauwezi kukufikia. Kumbuka, msaada wa Mwenrezi Mungu unategemea juu ya subira yako mwenyewe, kama vile wasiwasi inafuatwa na utulivu na dhiki inafuatwa na faraja.

36. Na omba ghofira na msaada wa Mwenyezi Mungu zaidi ya mara sabini kila siku.
37. Mtu anayetubia kwa dhambi zake amefanana na mtu asiye na dhambi.

## SOMO LA ISHIRINI NA MOJA MAAGIZO YANAYOMLAZIMU KILA MWISLAMU

Dhambi ni sumu msiimeze. 'Na kumwasi Mungu ni kifo kibaya kiogopeni. Ombeni ili mpewe nguvu. Sikilizeni! Mtu asiefahamu kuwa Mwenyezi Mungu ana uwezo juu ya kila kitu wakati wa kuomba kwake hayumo katika wafuasi wangu. Mtu asiyeacha kuzua na kudanganya hayumo katika jamaa yangu. Mtu mwenye kushughulika katika tamaa ya dunia, wala hainui macho yake kutazama mambo ya Akhera hayumo katika jamaa yangu. Mtu asiyetanguliza dini juu ya dunia kweli kweli hayumo katika jamaa yangu. Mtu asiyeacha kila kitendo kibaya kama kunywa pombe na kucheza kamari na kuzini na hiyana na rushwa, na kila jambo lisilojuzu kutenda na asiyetubia kutubu kwa kweli, hayumo katika jamaa yangu.

Mtu asiyedumu katika kusali sala tano siku zote hayumo katika jamaa yangu. Mtu asiyeshughulika katika kuomba kwa daima, wala hamkumbuki Mwenyezi Mungu siku zote kwa unyenyekevu, hayumo katika jamaa yangu. Mtu asiyeacha rafiki mbaya mwenye kumwingiza katika moyo wake mambo mabaya hayumo katika jamaa yangu. Mtu asiyeheshimu wa zazi wake wala asiyetii amri zao njema zisizo kinyume cha Kurani Takatifu, wala hawatumikii kwa haki hayumo katika jamaa yangu. Mtu asiyefanya wema kwa mke wake na jamaa za mke wake kwa upole na hisani hayumo katika jamaa yangu.

Mtu mwenye kumnyima jirani yake hata heri kidogo hayumo katika jamaa yangu. Mtu asiyetaka kumsamehe mwenye kosa kwake, na ni mwenye bughudha hayumo katika jamaa yangu. Kila mume mwenye kufanya hiyana kwa mke wake na kila mke mwenye kufanya hiyana kwa mume wake, hayumo katika jamaa yangu. Mtu anayevunja ahadi aliyoa hidi wakati wa kukiri na kuingia katika jamaa Ahmadiyya kwa sababu yo yote hayumo katika jamaa yangu. Mtu asiyeamini kwa kweli kuwa 'mimi ni Masihi na Mahdi, Kiongozi na Mjumbe aliyeahidiwa' hayumo katika jamaa yangu. Mtu asiyejiweka tayari kunitii katika mambo mema hayumo katika jamaa yangu. Mtu anayekaa pamoja na watu walionikataa na kukubali maneno yao ya upinzani hayumo katika jamaa yangu.

Na kila mzinzi, fasiki, mwuaji, mwizi, mcheza kamari, haini mla rushwa, mnyang'anyi, mdhalimu, mwongo, mhadaa na mwenye kukaa na watu hawa wote" na mwenye kusingizia ndugu zake na dada zake na asiyeacha vitendo vyake vibaya, wala asiache kukaa na watu wabaya; hayumo katika jamaa yangu. Enyi wafuasi wangu! kumbukeni kuwa haya yote ni sumu na baada ya kuzila sumu hizi hamwezi kusalimika. Nuru na giza haiwezekani kutangamana mahali pamoja. Kila mtu mwenye kuwa na tabia ya upotovu wala si safi kwa Mwenyezi Mungu hawezi kupewa baraka inayopewa wenye mioyo safi.

*(Seyidna Ahmad).*

Iwapo unapenda kununua vitabu zaidi vya Dini ya Kiislamu au kwa maelezo zaidi ya mafundisho ya Jumuiya ya Waislamu wa Ahmadiyya, wasiliana na anuani iliyo karibu nawe kati ya hizi zifuatazo:

1. P. O. Box 376, Simu: 2110473 Dar es Salaam.
2. P. O. Box 1, Simu: 2603477 Morogoro.
3. P. O. Box 260, Simu: 2646849 Tanga.
4. P. O. Box 359 Iringa. Simu 2700633.
5. P. O. Box 196, Simu: 243043 Dodoma.
6. P. O. Box 94, Simu: 2600847 Songea.
7. P. O. Box 10723 Arusha.
8. P. O. Box 54, Simu: 2603291 Tabora.
9. P. O. Box 547 Ujiji - Kigoma.
10. P. O. Box 306, Simu: 2333919 Mtwara.
11. P. O. Box 86, Simu: 2510082 - Masasi.
12. P. O. Box 1812 Bukoba.
13. P. O. Box 28, Simu 70 Kibiti - Rufiji.
14. P. O. Box 391 Tarime.
15. P. O. Box 605 Ifakara.
16. P. O. Box 17 Kilosa.
17. P. O. Box 40554, Simu: 764226 Nairobi Kenya.
18. P. O. Box 97011, Simu: 492624 Mombasa Kenya.
19. P. O. Box 421, Simu 40269 Kisumu Kenya.
20. P. O. Box 77, Simu 52 Shianda Kenya.
21. P. O. Box 552 Limbe Malawi.